JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI

Namba za simu.
Mkuu wa Shule-**0752 692425**.
Makamu Mkuu wa Shule**0764 339667**.
Mwl. wa Nidhamu**0753 758544**

Shule ya Sekondari **KISHOJU**,
S.L.P 11, **MULEBA-KAGERA**
Tarehe **29/03/2022**.

Mzazi/Mlezi wa …….. (Jina la Mwanafunzi)
S.L.P……

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISHOJU HALMASHAURI YA WILAYA YA MULEBA MKOA WA KAGERA MWAKA 2022/2023.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya Sekondari Kishoju mwaka 2022 **Tahasusi ya**……...…….

Shule ya Sekondari **KISHOJU** ipo umbali wa kilometa 5 kusini mwa mji wa **MULEBA**. Usafiri wa pikipiki kutoka **MULEBA** mjini unapatikana katika kituo cha basi kwa sh 1,500/= mpaka 2000/=.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **05/09/2022**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe **05/09/2022** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **19/09/2022**. (piga simu ili kujua kama kuna mabadiliko ya tarehe ya kufungua).

A: KARO

Unatakiwa kulipa karo ya shule Tsh. 70,000/= kwa mwaka, au unaweza kulipa Tsh. 35,000/= kwa Muhula. Karo iwekwe kwenye **A/C Na.32001200049** jina la akaunti**ni MDC KISHOJU SECONDARYSCHOOL-NMB**

Pamoja na karo kuna michango inayotakiwa kulipwa katika akaunti iliyotajwa nayo ni:-

i. Tsh 20,000 kwa ajili ya taaluma
ii. Tsh. 15,000 kwa ajili ya huduma ya afya
iii. Tsh. 15,000/= Pesa yaUkarabati wa samani
iv. Tsh. 5,000/= ,Pesa ya tahadhari (Haitarudishwa)
v. Tsh. 6,000/= Pesa ya kitambulisho na picha
vi. Tsh 2,000/= Pesa ya nembo (**inalipwa mara moja**)
vii. Mchango wa posho ya wapishi, walinzi n.k Tsh. 30,000/=.
viii. Tsh. 20,000 pesa ya mitihani ya kujipima
ix. Tsh. 5,000 /= kwa ajili ya Umeme

MWANAFUNZI ATALIPA TSH. 188,000/= KWA MWAKA AU 153,000/= KWA NUSU MWAKA.

NB: MICHANGO YOTE YA SHULE ILIPWE BANK NA SIYO KUTUMA KWA NJIA YA SIMU.

(B) MAHITAJI YA KUJANAYO SHULENI.

Mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo:-

1. Jembe 1 na mpini ,Dekio(squeezer/drier) yenye mpini wake na reki 1, kwa ajili ya usafi. (hii ni kwa wasichana tu).
2. Fyekeo/ kwanja na brashi ngumu yenye mpini, squeezer yenye mpini kwa ajili ya usafi pamoja na kotama 1. (hii ni kwa wavulana tu)
3. Mfagio wa soft broom 1, na chelewa ndefu ya nje (fagio la wima) kwa wote.
4. Ndoo 2 ndogo zenye mifuniko.
5. Vifaa vya chakula: bakuli ,sahani, kikombe na kijiko pamoja na vifaa vya usafi binafsi mf: mswaki, dawa ya meno kubwa, dawa ya viatu kubwa, mafuta ya kujipaka kopo kubwa, sabuni za kufua na kuoga, kanda mbili/yebo na taulo.
6. ***Kwa wasichana***: pair moja ya kitenge, na vifaa kwa ajili ya usafi wakimaumbile.(kanga hairusiwi)
7. Ream 2za karatasi za A4 zilizoandikwa (***DOUBLE A PREMIUM***) kwa mwaka.
8. . Kokotoo la hesabu (Scientific Calculator) kwa wanaosoma Hesabu. (HGE, EGM)
9. Mathematical set kwa wale wanaosoma geografia na hesabu
10. Vitabu vya masomo ya tahasusi yake (orodha imeambatanishwa mwanafunzi atapaswa kuchagua kwa mjibu wa tahasusi yake.
11. Godoro lenye urefu futi 6 upana futi 2 ½.
12. Taa ya betri / sora kwa tahadhali ya umeme ukikatika. (ISIWE YA KUCHAJI KWENYE UMEME)
13. Faili la nailoni (plastic file) la kutunzia mitihani, mazoezi na majaribio.

Aidha kwa wanaotoka mbali na watakaopenda vifaa namba 1,4, 5,7,8,9 na 11 unaweza kuvipata ndani ya duka la Shule. Vilevile Mwanafunzi hatapokelewa endapo hatakuja na taa kwa tahadhari ya umeme ukikatika.

SARE YA SHULE.

Unatakiwa kuwa na mavazi yafuatayo;-

a) WASICHANA.

i. Sketi mbili nyeusi za marinda ya kuelekea upande mmoja upana wa marinda ni inchi mbili (**Knife edge)**iwe na marinda kumi Upana wa mkanda usizidi inchi mbili. Urefu wa sketi kutoka kwenye magoti iwe inchi kumi chini ya magoti, kitambaa kisichoonyesha.(transparent).
ii. Shati mbili nyeupe mikono mirefu aina ya tetron (Tomato), lenye vishikizo vya kawaida na mfuko mmoja upande wa kushoto.
iii. Soksi nyeupe jozi mbili. (isiwe stocking/ free style) medium size
iv. Tai moja rangi Nyeusi yenye mistari nyeupe
v. Sweta rangi ya zambarau yenye nembo ya shule.
vi. Viatu pair mbili rangi nyeusi vya kufunga kwa kamba (soli fupi) isiwe boot shoes
vii. T-shirt 2 rangi ya **Nyekundu** zenye kola za mstari **mweusi**na kwenye mikono, zenye nembo ya shule.
viii. Track suit rangi nyekundu kwa ajili ya usiku (isiwe ya kubana na isiwe ya kofia)
ix. Kamusi ya Kiingereza kwa kiingereza (**Advanced Dictionary**) (HGL , HKL)
x. Madaftari makubwa (**Counter Books** 7) kwa ajili ya masomo saba na kalamu za wino za kutosha.
xi. Njoo na shuka jozi mbili, blanketi moja na mto mmoja na foronya (Mashuka yawe **rangi ya pinki** na yawekewe alama kuondoa usumbufu wa kupotea). Pia aje na chandarua.
xii. **Kwa wanafunzi wa kiislamu** watatakiwa kuwa na sketi nyeusi ndefu mbili zenye malinda, jarabibi nyeupe na panjabi mbili nyeupe zenye urefu sawa na shati. Kwa shughuli za nje atatakiwa kuja na sketi mbili ndefu za rangi ya zambarau pamoja na jarabibi na Panjabi za rangi ya Nyekundu.
xiii. Kwa wanafunzi wengine utatakiwa kuwa na sketi mbili rangi ya zambarau (***ya kuiva***) yenye mshono wa marinda sawa na sketi ya darasani kwa ajili ya shughuli za nje.

b) WAVULANA.

i. Suruali mbili nyeusi zenye urefu wa kufunika kisigino lakini siyo kuikanyaga**(iwe inchi 19 mzunguko wa chini)** . iwe ya **HESHIMA. (isiwe ya kubana wala modo).**
ii. Shati mbili nyeupe (aina ya tomato) mikono mirefu, zenye vishikizo vya kawaida na mfuko mmoja upande wa kushoto.
iii. Mkanda mweusi wa ngozi upana usiozidi inchi mbili (**usiwe namadoido**)
iv. Vazi baada ya saa za masomo ni suruali nyeusi na T-shirt yenye nembo ya shule hivyo uwe na suruali mbili za ziada kwa ajili ya shughuli za nje.
v. Jozi 2 za viatu vyeusi vya ngozi visiwe buti. Viatu visiwe na madoido viwe na visigino vifupi na vyenye kufungwa kwa kamba.
vi. Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi.
vii. Tai moja kama ilivyoainishwa kwa wasichana
viii. Sweta rangi ya zambarau yenye nembo ya shule
ix. T- shirt2 rangi ya Nyekundu zenye kola kama ilivyoainishwa kwa upande wa wasichana.
x. Track suit rangi ya blue kwa ajili ya usiku (isiwe ya kubana na isiwe ya Kofia)
xi. Kamusi ya Kiingereza kwa kiingereza (**Advanced Dictionary**) (HKL, HGL)
xii. Kalamu za wino za kutosha
xiii. Madaftari makubwa (Counter Books 7) kwa ajili ya masomo saba.
xiv. Njoo na shuka pair mbili, Blanketi moja na mto mmoja na foronya (**Mashuka yawe yarangi ya Blue)** na yawekewe alama kuondoa usumbufu wa kupotea. Pia aje na chandarua

Shuka la kiamasai HALITAKIWI SHULENI.

SARE ZINZOPATIKANA KWENYE DUKA LA SHULE NI:-

S/No	AINA YA SARE	KIASI
1	SWETA	15,000
2	T-SHIRT 2	30,000
3	TAI	5,000
4	T-SHIRT YA MICHEZO	8,000

NB: Kama mzazi atakumbana na changamoto kuhusu rangi ya sare za shule zilivyotajwa tafadhali wasiliana na uongozi kabla ya kufanya manunuzi ili kuondoa usumbufu wa kuwa na aina ya nguo (sare) tofauti na inayotakiwa. Pia Mwanafunzi atakayeripoti na nguo ambazo hazikuainishwa katika famu hii atalazimika kuzirudisha nyumbani.

c) WOTE:

i. Nywele fupi zisizozidi sentimeta moja
ii. Hairuhusiwi kubadili ngozi (**kujichubua**)
iii. Rangi kwenye kucha, wanja, ina na urembo mwingine kwa wasichana ni marufuku.
iv. T-Shirt 1 ya michezo ya kawaida (shingo round) wasichana nyekundu na wavulana blue kwa ajili ya michezo awapo uwanjani. Aidha Tisheti hizo zisiwe na aina yoyote ya maandishi isiwe transparent. Isiwe na maandishi yoyote (plain T-shirt).
v. Aje na bukta ya michezo rangi nyekundu kwa wasichana na bluu kwa wavulana.
vi. Aje na viatu vya michezo (**Raba nyeupe**).
vii. Ili kuimarisha shughuli za michezo shuleni wanafunzi wanaokuja kujiunga na shule yetu waje na pea moja, jezi na bukuta(full jersey) kama ifuatavyo:-

KIDATO	AINA YA JEZI
HKL	Mancity (Blue bahari)
HGE	Simba (RED)
HGL	Taifa Star (Blue)
EGM	Barcelona (RED)- chilizi

viii. Aje na nakala ya cheti cha uraia na nakala ya hati ya matokeo yake ya kidato cha nne (muhimu).

SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE ZINAZOPASWA KUFUATWA NA MWANAFUNZI

Wakati wowote watu wanapoishi na kufanya kazi pamoja huwa hapana budi sheria na kanuni ziwekwe ili kurahisisha uhusiano mwema katika mwenendo wa wale wanaohusika. Sheria zifuatazo zimewekwa ili kusaidia mwanafunzi kujiepusha na mambo ambayo yanaweza kusababisha asihitimu masomo yake.

Sheria hizi ni nyongeza tu kwa zile ambazo ni sheria za nchi na mila zetu na ambazo kila mzalendo anapaswa kuzifuata.

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi atakapotakiwa na katika mahudhurio ya kila siku hapa shuleni kama vile masomo, mikutano, kazi za kuzalisha mali, michezo na shughuli nyinginezo zitakazoandaliwa na shule.
b) Kila mwanafunzi atavaa nguo rasmi za shule wakati wote awapo shuleni. Nguo hizo zishonwe kwa mtindo wa heshima ulioamuliwa mamlaka husika.
c) Kila mwanafunzi atatakiwa kujiheshimu mwenyewe na kuheshimu watu wote ndani na nje ya mazingira ya shule na kuonyesha adabu na utii muda wote.

d) Kila mwanafunzi atakuwa na wajibu wa kulinda na kuhifadhi mali ya umma isiharibike, ***akiaribu kwa uzembe atalazimika kulipa***.
e) Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kutembelea nyumba za starehe, vilabu vya pombe au baa pamoja na nyumba za wafanyakazi isipokuwa kwa kibali maalumu.
f) Utoro au uzururaji wakati wa masomo au wakati wa kazi za uzalishaji mali ni marufuku. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kukaa katika mazingira ya shule wakati wote wa masomo, hata baada ya masomo isipokuwa kwa kibali maalumu.
g) Lugha inayotumika shuleni ni kiingereza akibainika mwanafunzi anatumia lugha tofauti na hiyo atahadhibiwa.
h) Kila mwanafunzi atashiriki katika shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo pamoja na usafi wa mazingira kwa mujibu wa ratiba. Kutoshiriki kwa makusudi kwa kutumia visingizio/ujanja wa aina mbalimbali hautakubalika. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya kibali halali kutoka kwa Daktarikiwasilishwe siku ya kuripoti.
i) Hairuhusiwe kujihusisha na mapenzi Shule (uasherati) ukibainika utafutwa Shule mara moja

j) ***Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni*** kwa kisingizio chochote kile, kukiuka sheria hii ***MWANAFUNZI HATOPOKELEWA***. *Na atalazimika kuirudisha nyumbani*

Zingatia : Kwa mawasiliano kati ya mzazi na mwanafunzi zitumike simu za shule kwa siku za Jumamosi saa 11: 00 jioni – 12:00 jioni.

a. 0745 444051 Wavulana tu
b. 0659158589 Wavulana tu
c. 0754 615611 Wasichana tu
d. 0678 303471 Wasichana tu

Kwa dharula wasiliana na Mkuu wa Shule, Makamu na Mwalimu wa Nidhamu

MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i Wizi
ii Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
vi kufuga nywele au ndevu (nywele zinatakiwa kuwa sentimeta moja)
vii Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii Uvutaji wa sigara
ix Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
x kupata ujauzito au kutoa mimba
xi Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii Kusababisha au kupata mimba
xiii Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiv Kumiliki, Kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xv Kudharau bendera ya Taifa
xvi Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xvii Uharibifu wa mali za Umma kwa makusudi.

VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

a. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi namkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
b. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
c. Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali(.**mwanafunzi atakayekuja bila kujaza fomu hii hatapokelewa).**
d. Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutembelea mwanafunzi Shuleni pamoja na namba zao za simu. Mwanafunzi anaweza kutembelewa Jumapili ya mwisho wa mwezi tu kuanzia saa 4:00 asubuhi – saa 8:45 mchana.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

N.B; ***MWANAFUNZI ATAKUWA NA LIKIZO FUPI 2 KWA MWAKA NA LIKIZO NDEFU 02 KWA MWAKA HIVYO, MZAZI MLEZI UTAWAJIBIKA KUMSAFIRISHA MWANAO KUMTOA NA KUMRUDISHA SHULENI WAKATI WA LIKIZO ZOTE.***



P.W.KULWA
MKUU WA SHULE



Kwa mawasiliano zaidi tumia namba za simu zilizotajwa katika ukurasa namba 1.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Shule ya Sekondari Kishoju,

S.L.P 11,

MULEBA.

TAREHE: 29/03/2022

KIAMBATANISHO A: MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina Kamili la Mwanafunzi …….

2. Anwani ya nyumbani …….

3. **Mahali alipozaliwa**, (i) Wilaya……...
   (ii) Tarafa……...
   (iii) Kata ……..…
   (iv) Kijiji/Mtaa……..…

4. **(a) Shule ya Sekondari ulipotoka ……..**
   (b) Anwani ya Shule ulipotoka ……
   (c) Mwaka aliomaliza Shule ya Sekondari……..
   (d) Mchezo unaopendelea zaidi……

5. **Dini ……**

6. **Wazazi** (i) Jina la baba……..
   Anwani yake …….
   Namba ya simu ya mkononi …….
   Anaishi/ Amefariki (Kata isiyohusika)
   Saini……..
   (ii) Jina la mama ……....
   Anwani yake ……
   Namba ya simu ya mkononi …….
   Anaishi/ amefariki (kata isiyohusika)
   Saini……
   (iii) Jina la Mlezi (kama si baba au mama)
   Anwani yake …….
   Namba ya simu ya mkononi ……..
   Uhusiano wake na wewe ni ……....
   (iv) Saini ya Mlezi ……
   (v) Saini ya Mwanafunzi ……...

MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi …….. nakiri kwamba sitoshiriki katika mgomo wowote, fujo yoyote, kuhudhuria kikao kisicho na idhini ya utawala katika mazingira yote ya shule na kwamba sitoshiriki makosa yoyote ya jinai.
Nikiwa mwenye akili timamu naapa sitojihusisha na utovu wowote wa nidhamu na nitafuata taratibu/sheria, ratiba kwa mjibu wa mipango ya shule. Na sitazungumza kauli yoyote ya kuchochea/kuhamasisha/kushinikiza /kushawishi uvurugaji wa amani ya Shule mtu/kikundi/mdahalo.Sitashiriki majadiliano/maandamano/mabishano yanayohatarisha amani ya shule.
Ikiwa nitatenda kinyumena niliyotaja hapo juu niwajibishwe kwa mujibu wa sheria za shule.

Jina la ukoo…… Jina la kati……..….. Jina la kwanza ……

Sahihi …….. Tarehe…….……..

UTHIBITISHO WA MZAZI/ MLEZI
Mimi……Mzazi/mlezi
wa……..…(mwanafunzi) nathibitisha kwamba mwanangu amesoma na kuelewa mkataba huu. Akienda kinyume na mkataba huu asimamishwe masomo mara moja na atua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yyake.

Sahihi …… tarehe …… namba za simu……..

IJAZWE NA MZAZI/MLEZI NA KURUDISHWA SHULENI

ANWANI YA MLEZI
……
……
TAREHE……

KUMB NA……..
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KISHOJU
S.L.P. 11
MULEBA.

YAH: MALEZI YA MTOTO ……..KIDATO CHA…….……TAHASUSI YA ……MWAKA……

NIMEZISOMA SHERIA NA Kanuni za shule Kumb.Na.KSS/02 na kuzielewa.
Ninapenda kuhakikisha kwamba mimi mzazi/mlezi wa mtoto huyo /niko tayari kusaidiana na shule katika jitihada zote za kumjengea mtoto wangu nidhamu ya dhati wakati wote awapo shuleni
Naahidi nitajitahidi kumwongoza kwenye masomo yake kulingana na taratibu za shule.

ZINGATIA:

i. Asikose kuhudhuria shuleni kama hakuna sababu ya msingi ya kumzuia na akikosa, apewe kibali toka kwa mzazi/mlezi wake bila hivyo hatapokelewa.
ii. Asijihusishe na matendo ya utoro , uzururaji, matumizi ya madawa ya kulevya na vitendo vinginevyo ambavyo vinaweza kumzuia kuendelea na shule.
iii. Asipuuze au kukataa kuhudhuria miradi ya shule , kama vile kilimo na kutunza usafi wa mazingira.
iv. Asijihusishe na migomo au ushawishi wowote unaoweza kuvunja amani ya shule kwani kwa kufanya hivyo atafukuzwa shule mara moja.
v. Akazanie masomo kwa lengo la kufaulu mitihani yake ya ndani nayanje.

…… ……
JINA KAMILI MZAZI/MLEZI **SAHIHI**

MEDICAL EXAMINATION FORM DATE……

NAME OF STUDENT……..

To medical office I/C of …….District/Regional;/Referral/Designated Hospital: P.O.BOX …….

Please examine the above named in full as to his/he physical and mental fitness for Being able to pursue years of Secondary school Education. In case of an acute Defect/disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs:-

i. Blood pressure ……

ii. Sickle cell test …….

iii. (a) Eyesight ……..…
(b) Hearing ……...

(c) Spleen …….

(d) Limps …….

(e) Venereal diseases ……

(f) Leprosy…….

(g) Epilepsy……..…

(h) Typhoid ……..

iv. Neuroses ……...
v. Other serious diseases…….…..
vi. Pregnancy:……

General comment (s)……

Name…….Signature……..
Designation …….
Official stamp……..
Date …….

ANGALIZO:Mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina na sahihi ya mganga .Atakayegundulika shuleni kuwa hakuchukuwa vipimo kihalali atarudishwa nyumbani.

ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI

EGM:

1. GS

Bigirwamungu J and Deogratias MS (2015), ***Understanding Advanced level General Studies***

2. ECONOMICS

a. Ambilikile C(2009), ***Advanced Economy Book 1***
b. ***A straight heard economics Edition for high level students book 02. By Zist Kamili***

3. GEOGRAPHY

D.T.Msabila (2014), ***A comprehension of physical Geography for secondary school. New Edition***

4. MATH'S

a. Mathematics; class xi, class xii volume 1&2, by chande and Pure Mathematics 1&2.
b. Sillem S.I (2015) Advanced Mathematics for Advanced secondary School form V. Dar es Salaam EDY publisher
c. Sillem SI. (2015). Advanced mathematics for Advanced secondary school form VI Dar. Es Salaam GDY publisher
d. Dass H.K Verma (R.6th Edition 2015) Mathematics for class X11 volume I. New Delhi S.Chand & company LTD.
e. Crawshaw, J& Chambers J. (1994). A concise course in A – level statistics with worked Examples 3rd Ed. London.
f. Bostock, L Chandler S (1978) Pure mathematics 1 London: Stanley Thornes Publishers Ltd.
g. Bundary B.D Malholland H. (1970) Rev Pure Mathematics for Advanced level, London Buther worth & Co. publisher LTD.

HGE

1. GS

a. Bigirwamungu J and Deogratias MS (2015), ***Understanding Advanced level General Studies***
b. ***Zist Kamili 2 (2017) straight forward general & Development studies.***

2. HISTORY

a. Shibitali, C.K.T (2012),***Contemporary Historical Events, Advanced level History two.***
b. ***Mwl. Kato, (2009) A mastering Advanced level History 1 &2***
c. Shibitali, C.K.T (2010), ***Contemporary Historical events, Advanced level History one.***
d. *Yasin, S (2010) Essentials in Advanced Level History Paper 2 Dar es Salaam TZ,*
e. Bigirwamungu I and Deogratius.M (2015)***Understand African History paper 1***

3. BAM :

a. ***Sillem S.I (2014) Basic applied mathematics for form VI. Dar es salaam GDY publisher.***
b. ***Sillarm S.I (2015) Basic applied mathematics for form VI. Dar es Salaam GDY publisher.***

4. GEOGRAPHY

a. D.T.Msabila (2014), ***A Comprehension of physical Geography for secondary school New Edition***
b. Zist Kamili (2010) geography II Alive Human and Economic Geography

5. ECONOMICS:

a. Ambilikile. C (2009), ***Advanced Economy Book 1***
b. ***Zisti Kamili a straight forsed Economics edition for high school standards book 01***

HGL

1. HISTORY

a. Shibitali, C.K.T (2012),***Contemporary Historical Events, Advanced level History two.***
b. Shibitali, C.K.T (2010), ***Contemporary Historical events, Advanced level History one.***
c. Bigirwamungu I and Deogratius. M (2015),***Understand African History paper 1.***

2. GEOGRAPHY

a. D.T.Msabila (2014***), A Comprehesseion of physical Geography for secondary school New Edition.***
b. Zisti, Kamili (2010) The Earth's physical Environment Physical Geography Aline

3. ENGLISH

Ashel.N(2010); Advanced level English Language. A practical Aproach. Dar es Salaam. Good Books publishers.

4. GS

Bigirwamungu J and Deogratias MS (2015), ***Understanding Advanced level General Studies***

HKL

1. GS

Bigirwamungu J and Deogratias MS (2015), ***Understanding Advanced level General Studies***

2. KISWAHILI

Christopher M(2016), ***Nadharia ya Lugha Kidato cha V na VI***

3. HISTORY

a. Shibitali, C.K.T (2012) ***Contemporary Historical Events, Advanced level History two.***
b. Shibitali, C.K.T (2010***), Contemporary Historical events, Advanced level History one.***
c. Bigirwamungu I and Deogratius. M (2015***) Understand African History paper 1.***

4. ENGLISH

a. Ashel. N(2010); ***Advanced level English Language. A practical Aproach.*** Dar es Salaam. Good Books publishers.
b. Betrayal in the city An enemy of the people
c. The Beautiful ones Are Not yet Born
d. Aman of the people
e. Lwanda Magere

NB: Mwanafunzi anatakiwa kuwa na vitabu vyote kwa mjibu wa combination yake hata kama kitabu hakikutajwa kwenye combination husika.

SCHOOL MOTTO: AIM HIGHER